Kwa kuwa vitabu vya kiada ndivyo vinavyo beba mada za isimu, ni dhahiri kuwa upungufu mkubwa wa vitabu unasababisha wanafunzi wasiandaliwe vema kumudu somo la isimu Chuo Kikuu. Warming (1982) anasema kwamba vitabu vya kiada ni chanzo muhimu kwa mwanafunzi shuleni kwa ajili ya kujifunza, kueneza utamaduni, na kuongeza maarifa ya wanafunzi. Msanjila (2005) anasema kuwa kutonunuliwa vitabu vya kutosha vya Kiswahili sekondari ni ishara mojawapo kuwa somo la Kiswahili halipewi kipaumbela kama yalivyo masomo ya sayansi na kiingereza.

Warning (1982) akiwarejea Edge na Wharton (1998) na Tomlinson (2008) anasema kuwa vitabu vya kiada yafaa viwe msaada kwa ajili ya mwalimu ambaye si mzoefu, au walimu wasio wazoefu katika ufundishaji wa lugha, hasa lugha ya mazungumzo.

### 4.4.1.6 Upungufu Uliomo Katika Mtaala wa Kiswahili Sekondari Ni Kikwazo Katika Kuwaandaa Vema Wanafunzi Wanaosoma Kiswahili Sekondari

Maswali namba 10 na 11 kwa ajili ya wanaChuo yalilenga kubaini upungufu uliomo katika mtaala wa sekondari ambao huchangia mada kadhaa kutowaandaa vema wanafunzi wanaohitimu somo la Kiswahili sekondari kwenda kusoma somo la isimu vyuo vikuu. Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu wanne kati ya watano sawa na 80% na kwa walimu lilikuwa swali namba 17, ambapo walimu wa Kiswahili sekondari 11 kati ya 14 sawa na 78.6% ya waliojibu swali hili walitaja upungufu ufuatao:-

i) Mtaala hautilii mkazo mada za isimu katika ngazi ya sekondari ndio maana hakuna vitabu vya kiada vya isimu ilhali sekondari kuna vitabu vya kiada vya fasihi kwa kidato cha tatu hadi cha sita

ii) Vitabu vya rejea vya isimu havitoshi kwa wanafunzi na vina viwango vya elimu ya juu zaidi.

iii) Fasili ya Mofimu na uchanganuzi wa tungo haviendani na vyuo vikuu.

iv) Fonetiki, fonolojia na isimujamii hazimo katika mtaala wa sekondari.

v) Hakuna maabara za masomo ya lugha.

vi) Hakuna walimu wenye ujuzi wa isimu, wanategemea vitabu vya kiada ambavyo hutofautiana na hivyo kuwachanganya walimu na wanafunzi.

vii) Kuna baadhi ya mada hazimo katika mtaala lakini maswali yake hutokea kwenye mitihani.

viii) Kuna baadhi ya mada hazimo katika muhtasari lakini zimo katika vitabu vya kiada.

ix) Baadhi ya vitabu vya kiada huhitilafiana kimaudhui hivyo kuleta mkanganyiko.

x) Mada hazina mpangilio unaoeleweka bali hujirudia katika vidato vya juu.

xi) Uainishaji wa ngeli za nomino yafaa uwe na kigezo kimoja.

xii) Mipaka ya mofimu kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili si bayana.

xiii) Hakuna semina za mada za isimu.

xiv) Vitabu vya kiada na kamusi shuleni havitoshi.

xv) Kuwe na kitabu rasmi kwa ajili mada za isimu tu.

Maelezo yao hayo yanajibu swali lililotaka kujua mada za sekondari zisizowaandaa veema kumudu somo la isimu vyuo vikuu. Upungufu namba (i) mpaka (xv) ni sehemu ya upungufu wa mtaala mchanganyiko ambao husababisha wahitimu wa sekondari kwa mada za isimu wasiandaliwe vema kusoma kwa ajili ya kwenda kusoma somo la isimu Chuo Kikuu.

Kwa mujibu wa data kutoka maktabani, upungufu kama huo ulibainishwa pia na Msanjila (2005), Ndosi (2011), Mtana (1998) na Mbalamwezi (2012).

#### 4.4.1.7 Zipo Mada Za Isimu Sekondari Ambazo Zina Msaada Kwa Mwanafunzi Atakayekwenda Kusoma Isimu Chuo Kikuu

Swali la nne la hojaji liliwataka wanafunzi wa Chuo Kikuu walinganishe namna mada za sekondari zilivyowasaidia kujifunza kozi mbali mbali za isimu. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

**Jedwali 4.2: Namna Mada Za Sekondari Zilivyowasaidia Kujifunza Kozi Za Isimu Chuo Kikuu**

| **Jina la kozi** | **Idadi ya watafitiwa** | **Zimesaidia sana** | **Zimesaidia** | | **Zimesaidia kidogo** | | **Hazijasaidia kabisa** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| Fonetiki | 5 | 0 | | | | | 05 | 100% |
| Fonolojia | 5 | 0 | 02 | 40% | 03 | 60% | | |
| Mofolojia | 5 | 0 | 04 | 80% | 01 | 20% | | |
| Sintaksia | 5 | 0 | 03 | 60% | 02 | 40% | | |
| Semantiki | 5 | 0 | 02 | 40% | 03 | 60% | | |
| Isimujamii | 5 | 0 | | | 02 | 40% | 03 | 60% |

Chanzo: Data kutoka uwandani (2016)

Jedwali namba 4.2 hapo juu linashabihiana na jedwali 4.1 kwasababu linaonesha kuwa fonetiki bado inaongoza kwa kutokuwa na kozi tangulizi zinazoweza kumsaidia mwanafunzi atakayehitimu Kiswahili sekondari na kwenda kusoma isimu Chuo Kikuu. Kwa upande mwingine mofolojia (80%) inaonekana ikiwa na mada tangulizi nyingi na hivyo kuwa msaada mkubwa kwa mwanafunzi atakayekwenda kusoma isimu Chuo Kikuu, ikifuatiwa na mada ya sintaksia (60%) ambazo zimo kwenye kipimo cha zimesaidia. Mada hizo ni msaada kwa mwanafunzi aliyehitimu Kiswahili sekondari na kwenda kusoma isimu Chuo Kikuu. Ni dhahiri kuwa wanafunzi hupata shida sana kwa kukosa mada tangulizi kwa ajili ya kujifunza kozi ya fonetiki na fonolojia Chuo Kikuu. Matokeo haya yanajibu lengo mahususi la kwanza kwamba zipo mada kadhaa zinazowaandaa vema wanafunzi wa sekondari kama mada zinazohusiana na mofolojia na sintaksia na zile ambazo haziwaandai vema kujifunza kozi ya isimu vyuo vikuu kwa mfano mada zinazohusiana na kozi ya fonetiki na fonolojia kama ilivyooneshwa kwenye jedwali (na. 4.2) hapo juu.

### 4.4.2 Maoni Hasi Dhidi Ya Mada Za Isimu Na Somo La Kiswahili Kwa Ujumla

Utafiti huu pia ulichunguza maoni hasi ya wanafunzi na walimu kuhusu mada za isimu na zisizo za isimu kwa sababu hii inaweza kuathiri ujifunzaji, umilisi wa sarufi na mazungumzo (Babusa, 2010).

#### 4.4.2.1 Wanafunzi Hutenga Muda Mfupi Wa Kusoma Mada Za Isimu

Swali la 7 lililenga kubaini jinsi wanafunzi wa sekondari wanavyotenga muda wa kusoma mada za isimu zikilinganishwa na mada nyinginezo, ambapo sarufi na utumizi wa lugha vililinganishwa na fasihi simulizi, riwaya, na uandishi. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

i) Sarufi na utumizi wa lugha = wanafunzi 05,

ii) Fasihi simulizi= wanafunzi 09,

iii) Riwaya na Tamthiliya (R&T) = wanafunzi 18,

iv) Uandishi = wanafunzi 02.




**Kielelezo 4.7: Namna Wanafunzi Wanavyotenga Muda Wa Kusoma Mada Mbali Mbali Za Somo La Kiswahili Sekondari**

Muda ambao mwanafunzi anatenga kwa ajili ya kusoma mada kwa siku ni ishara ya jinsi mwanafunzi anavyothamini mada husika. Mada anazozipenda mwanafunzi huzitengea muda mwingi zaidi. Kudhani kuwa mada au somo usilolitengea muda wa kutosha utalifaulu ni sehemu ya mtazamo hasi wa mada hiyo au somo hilo.

Kuhusu umuhimu wa kutenga muda wa kutosha kwa somo linalothaminiwa, Msanjila (2015) anasema kuwa inashangaza kuona kuwa somo la Kiingereza limetengewa vipindi sita kwa juma ilhali somo la Kiswahili limetengewa vipindi vitatu tu.

#### 4.4.2.2 Maoni Hasi Ya Wanachuo Kuhusu Mada Za Isimu

Maswali namba 6 hadi 8 yalilenga kubaini maoni hasi kwa wanaChuo kuhusu mada za isimu na somo la Kiswahili ambalo kwa sekondari limebeba pia mada za isimu. Swali hili ni la msingi kwa kuwa kama wanafunzi wana mtazamo hasi dhidi ya mada za isimu au somo la Kiswahili, au hata jamii kwa ujumla ina mtazamo hasi ni dhahiri kuwa wanafunzi hawatasoma kwa moyo mkunjufu isimu ambayo ni sehemu pia ya somo la Kiswahili katika shule za sekondari. WanaChuo walitakiwa waeleze hadhi ya mwalimu wa sayansi akilinganishwa na mwalimu aliyesoma Kiswahili. WanaChuo walikuwa na haya ya kusema:-

i) Serikali inathamini masomo ya sayansi zaidi kwa kuwa hata wanaopewa mikopo vyuo vikuu ni wale wanaosoma masomo ya sayansi

ii) Somo la Kiswahili linachukuliwa kuwa ni rahisi na mtu yeyote anaweza kulisoma hata mwenye akili ya chini

iii) Wanaosoma sayansi hudhaniwa kuwa ni wabunifu zaidi

iv) Somo la Kiswahili hudhaniwa kuwa ni somo la wanawake

v) Wakilinganisha mada za fasihi na isimu (swali namba 8) wanafunzi wote watano sawa na 100% walisema mada za isimu ni ngumu kuliko mada za fasihi. Wakihitimisha walisema kuwa katika mitihani ya NECTA wanafunzi wengi hufaulu fasihi zaidi.

Swali hili linajibu lengo la pili lililotaka kubaini mtazamo hasi wa walimu na wanafunzi kuhusu mada za isimu zilizomo katika mtaala wa Kiswahili. Imedhihirika kuwa wanafunzi wanaamini kuwa Kiswahili hakina hadhi kubwa kama masomo mengine hasa ya sayansi na kwa hali hii wana mtazamo hasi dhidi ya somo la Kiswahili ambalo kwa shule za sekondari hujumuisha mada za isimu.

Kwa mujibu wa data kutoka maktabani, swala la mtazamo hasi wa somo lilibainishwa pia na Seka (1979) katika tasnifu yake ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Seka alitafiti kuhusu mambo yanayoathiri ufaulu mzuri katika somo la hisabati miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha nne katika shule za sekondari nchini Tanzania. Miongoni mwa mambo aliyoyabainisha ni pamoja na wanafunzi kuwa na imani potofu kuwa hesabu ni ngumu. Katika maoni ya wanaChuo hapo juu (v) tumeona pia wakisema kuwa mada za isimu ni ngumu. Pia mtazamo hasi wa mada zilizo ndani ya somo la Kiswahili umewahi kubainishwa na Mbunda (1979), alibaini kuwa wanafunzi walikuwa na mtazamo hasi wa somo la Kiswahili ndiyo maana walikuwa hawafanyi vizuri katika mada ya uandishi. Matokeo ya utafiti huo yana uhusiano na utafiti huu kwa kuwa alichunguza ufundishaji wa mojawapo ya mada iliyojumuishwa ndani ya somo la Kiswahili sekondari, ambapo katika utafiti

wa Mbunda na utafiti huu, zote zimebainisha mtazamo hasi wa wanafunzi dhidi ya somo la Kiswahili ambacho kimebeba mada zilizokuwa zinachunguzwa.

Hoja namba (iv) hapo juu kuwa Kiswahili hudhaniwa ni somo rahisi ni mtazamo hasi ambao una ufanano na maelezo ya utafiti wa Msanjila (2005) anaposema kuwa inapotokea kuwa shule haina mwalimu wa Kiswahili, mkuu wa shule huweza kuteua mwalimu yeyote afundishe somo hilo hata kama si mwalimu wa somo la Kiswahili. Msanjila anaongeza pia kuonesha jinsi Kiswahili kisivyothaminiwa kwa kutokuwa na semina za mara kwa mara za walimu wa somo hilo na pia kutotengewa fedha nyingi za kununulia vitabu vya Kiswahili na vifaa vya kujifunzia kama yalivyo masomo ya sayansi, Kiingereza na hisabati. Katika mtazamo hasi wa somo la Kiswahili wa namna hiyo somo la isimu ambalo ni sehemu ya somo la Kiswahili sekondari haliwezi kuwa na msingi mzuri kwa wanafunzi watakaokwenda kusoma isimu Chuo Kikuu. Katika sehemu ya (V) hapo juu watafitiwa wameonesha mtazamo hasi dhidi ya isimu kuwa ni ngumu madai ambayo msingi wake haujafahamika.

#### 4.4.2.3 Maoni Hasi Ya Wanafunzi Wa Sekondari Dhidi Ya Mada Za Isimu Kwa Kulinganisha Na Mada Nyinginezo za Kiswahili

Swali namba mbili kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma sekondari lilikusudia kubaini mada ya Kiswahili zinazochukiwa zaidi na wanafunzi. Mada zilizolinganishwa zilikuwa; fasihi simulizi, sarufi, fasihi andishi, na maendeleo ya Kiswahili. Lengo la swali hili lilikuwa kupima kiwango ambacho wanafunzi wana mtazamo hasi kwa mada za isimu. Pia swali la tatu liliwataka waeleze sababu zilizowafanya wachague

mada kuwa ya kwanza kwa kuipenda. Matokeo yamewasilishwa katika jedwali lifuatalo. Wanafunzi wote 34 walijibu swali hili kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.3**: **Maoni Hasi Dhidi Ya Mada Za Isimu**

| **Mada** | **Jumla ya washiriki** | **Walioipenda zaidi kwa kuweka 1** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Fasihi simulizi | 34 | 15 | 44.1% |
| Sarufi | 34 | 04 | 11.8% |
| Fasihi andishi | 34 | 09 | 26.5% |
| maendeleo ya Kiswahili | 34 | 06 | 17.6% |
| | | Jumla | 100% |

Chanzo: Data kutoka uwandani (2016)

Jedwali hapo juu linaweza kuoneshwa vizuri katika kielelezo cha pia kifuatacho:




| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia | 44.1% | 11.8% | 26.5% | 17.6% |

**Kielelezo 4. 8: Mtazamo Hasi Dhidi Ya Mada Za Isimu**

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2016). Ufunguo: Asilimia ndogo=mtazamo hasi

Kutokana na jedwali namba 4.3 na kielelezo cha pia namba 4.8 hapo juu, imedhihirika kuwa wanafunzi wengi wanamtazamo hasi dhidi ya mada ya sarufi

ambayo ni mada iliyo katika kozi ya isimu. Kama wanafunzi wengi wana mtazamo hasi dhidi ya mada ya sarufi si rahisi mada hiyo ikawaandaa vema kwa ajili ya kusoma isimu Chuo Kikuu. Mtazamo hasi wa mwanafunzi humfanya ashindwe kujifunza vizuri somo au mada husika kama asemavyo Seka (1979), Mbunda (1979) na Babusa (2010).

#### 4.4.2.4 Maoni Hasi Kwa Mada Za Kiswahili Isimu, Kuhusu Mada Za Kiswahili Ambazo Wangepaswa Kuendelea Nazo Vyuo Vikuu

Swali la 5 liliwataka wanafunzi wa sekondari wachague mada moja kati ya nne ambazo wangependa kuendelea nazo katika elimu ya juu. Mada zilizowasilishwa kwao ili wachague zilikuwa:

a) Fasihi andishi.

b) Fasihi simulizi.

c) Sarufi na utumizi wa lugha, na

d) Ushairi.

Matokeo ya swali hilo ambalo lilijibiwa na wanafunzi wote 34 yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.4: Maoni Hasi Dhidi Ya Mada Za Isimu**

| **Mada** | **Washiriki** | **Mada ya kuendelea nayo elimu ya juu** | **%** |
|---|---|---|---|
| a) Fasihi andishi | 34 | 09 | 26.5% |
| b) Fasihi simulizi | 34 | 16 | 47.1% |
| c) Sarufi na utumizi wa lugha | 34 | 03 | 08.8% |
| d) Ushairi | 34 | 06 | 17.6% |
| | | Jumla | 100% |

**Ufunguo: Asilimia ndogo=Maoni hasi. Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2016)**

Mada za isimu hata pale zilipolinganishwa na mada nyinginezo za Kiswahili pamoja na fasihi simulizi bado matokeo yalionesha vile vile. Kwa hakika mada za isimu zimekosa mizizi kiasi cha kutopendwa tangu sekondari na hivyo kuwafanya wasiwe na utayari wa kusoma isimu vyuo vikuu. Kwa hakika wanafunzi wana mtazamo hasi dhidi ya mada za isimu. Kwa hiyo imedhihirika kuwa wanafunzi wa sekondari wana mielekeo hasi dhidi ya mada za isimu.

Jedwali hapo juu linaweza kuoneshwa vizuri katika kielelezo kifuatacho:




| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia | 26.5% | 47.1% | 08.8% | 17.6% |

**Kielelezo 4.9: Maoni Hasi Ya Wanafunzi Dhidi Ya Mada Za Isimu**

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2016)

Matokeo haya kama ilivyo jedwali namba 4.4 hapo juu yanaonesha kuwa wanafunzi wengi wangependa waendelee na somo la fasihi katika elimu ya juu. Hivyo mada za isimu haziwavutii wanafunzi walio wengi wanapojifunza somo la Kiswahili

sekondari na kwa vyovyote vile haziwezi kuwaandaa vema kusoma isimu vyuo vikuu wakati wamekwisha zichukia kuanzia ngazi ya elimu ya sekondari.

Wakijibu swali la sita lililowataka kutoa sababu za chaguo walilolifanya katika swali la tano hapo juu; waliochagua fasihi simulizi ambazo ni 47.1% walikuwa na haya ya kusema:

i) Mwalimu anapofundisha hueleweka vizuri.
ii) Inaelimisha na kufurahisha.
iii) Inasaidia kufikisha ujumbe kwa jamii.
iv) Ina uhalisia katika maisha ya kila siku.
v) Siyo ngumu kueleweka.

Tunaona mtazamo hasi wenye imani potofu kuwa mada za isimu ni ngumu ukiendelea kutajwa na wanafunzi wa sekondari walio wengi pia kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu. Matokeo yalidhihirisha kuwa fasihi simulizi na fasihi andishi, ndizo stadi zilizopendelewa sana na wanafunzi zikifuatwa na fasihi andishi.

Katika utafiti wa Njogu (2015) alibaini kuwa, stadi zilizokosa umaarufu miongoni mwa wanafunzi zilikuwa sarufi na matumizi ya lugha zikiwa na wastani wa 2.30 na kuandika ikiwa na wastani wa 1.70. Njogu (2015) alihitimisha kwa kusema kuwa matokeo hayo yalikuwa ya kusikitisha kwani sarufi ni muhimu sana katika kujenga umilisi wa lugha. Anamnukuu Williams (2005) ambaye anasema kuwa sarufi huathiri umilisi wa kuandika, Njogu anasema kuwa hoja hii inaungwa mkono na Gathumbi na Masembe (2005) na Bwire na Vikiru (2008).

#### 4.4.2.5 Mgawanyo Mbaya Wa Alama Katika Mitihani ya NECTA Husababisha Maoni Hasi

Maswali namba 6 hadi 8 ya mahojiano kwa walimu na wakuu wa idara za Kiswahili yalijibiwa na wakuu wa idara wote 7 na walimu wa Kiswahili 14 sawa na 100%. Maswali yalikusudia kubaini mtazamo hasi kwa mada za isimu unaochangiwa na maelekezo ya mitihani ya NECTA. Ulinganisho ulifanywa katika mgawanyo wa alama za mitihani ya kitaifa kwa mada zinazohusu isimu na mada zisizo husu isimu. Lengo la ulinganisho huo lilikuwa kubaini mada ambazo zimetengewa asilimia kubwa ya alama kwa upande wa mitihani ya kitaifa. Kwa ujumla watafitiwa wote 21sawa na 100% walikiri kuwa mada zinazohusu isimu zilikuwa na alama ndogo katika mitihani kitu ambacho huwanyima motisha wanafunzi na walimu wa sekondari hivyo kutotilia mkazo mada za isimu.

Mtazamo hasi huweza kusababishwa na ukosefu wa motisha wa alama katika mitihani ya kitaifa kama asemavyo Njogu (2015) anapo wanukuu Gathumbi na Masembe (2005) kuwa wanafunzi wengi huimarisha lugha tu kwa minajili ya mitihani na wakisha kuifanya mitihani hiyo hupuuzilia mbali kanuni faafu za lugha hiyo na hata kuichukulia kama wasiyoielewa kabisa. Kwa kauli hiyo ni dhahiri kuwa kama mada haina alama nyingi kwenye mtihani wa mwisho kama ilivyo mada za isimu si wanafunzi wala walimu wanaoweza kuwa na mtazamo chanya dhidi ya mada hizo.

Kwa mujibu wa data toka maktabani; kwa mitihani ya taifa ya kidato cha nne kwa miaka mitatu mfululizo (2013-2015); mgawanyo wa alama kwa mada zote ni kama

**ifuatavyo:**

**Jedwali 4.5: Sarufi na Utumizi wa Lugha Zina Alama Ndogo**

| **Mada** | **Sehemu** | **Alama Katika %** |
|---|---|---|
| Ufahamu | A | 10 |
| Sarufi Na Utumizi Wa Lugha | B | 25 |
| Uandishi | C | 10 |
| Maendeleo Ya Kiswahili | D | 10 |
| Fasihi Kwa Ujumla | E | 45 |
| **Jumla Ya Alama** | | 100 |

Chanzo: Mitihani ya NECTA (2013-2015)

Kutokana na Jedwali hilo, ni dhahiri kuwa mwanafunzi akifaulu *fasihi kwa ujumla* (sehemu C) atapata ufaulu wa C (45%), ilhali akifaulu *fasihi na utumizi wa lugha* (sehemu B), alama yake ya ufaulu itakuwa F (25%). Hivyo lazima awe na mtazamo hasi dhidi ya mada za isimu zilizomo katika sehemu B(Sarufi na utumizi wa lugha). Halikadhalika kwa mwalimu anayetaka wanafunzi wake wafaulu, nguvu yake kubwa hataielekeza kwenye Sarufi na utumizi wa lugha.

### 4.4.3 Njia Zinazoweza Kutumika Ili Wanafunzi Wamudu Vema Mada za Isimu Sekondari na Hatimaye Vyuo Vikuu

#### 4.4.3.1 Mapendekezo ya Wanachuo Kuhusu Uimarishaji wa Isimu Sekondari

Katika swali la 11 wanafunzi wa Chuo Kikuu walipendekeza yafuatayo yafanyike ili kukuza isimu sekondari na hatimaye vyuo vikuu.

i) Mada za utangulizi kwa ajili ya kozi za fonetiki, fonolojia na isimujamii ziingizwe katika mtaala wa sekondari kwa kiasi cha kuweza kumsaidia mwanafunzi atakaye kwenda kusoma isimu Chuo Kikuu

ii) Vitabu vinavyoshughulikia isimu tu viandaliwe kwa ajili ya shule za sekondari.

iii) Maabara za lugha ya Kiswahili zianzishwe

iv) Mada zipangwe vizuri na kwa kufuata vidato

v) Kwa baadhi ya mofimu, mipaka baina ya mofimu haiko wazi, yafaa zipewe tahajia mpya.

#### 4.4.3.2 Mapendekezo ya Walimu Wa Sekondari Pamoja Na Wakuu Wa Idara Za Kiswahili Sekondari Kuhusu Uimarishaji Wa Isimu

Asilimia 78.6% ya walimu wa somo la Kiswahili waliojibu swali namba 18 na wakuu wa idara za Kiswahili sekondari wote 7 waliojibu swali namba 16 la mahojiano lilowataka wataje jinsi ya kupunguza matatizo yaliyomo katika mtaala wa sekondari yanayokwamisha ujifunzaji mzuri wa mada za isimu sekondari yanavyoweza kuondolewa au kupunguzwa walikuwa na mapendekezo yafuatayo:-

i) Kuwepo na kigezo maalumu cha kutambua aina za sentensi

ii) Kuwe na kigezo kimoja cha upatikanaji ngeli

iii) Maneno yaandikwe vizuri ili iwe rahisi kuzigawa mofimu

iv) Kuwe na kitabu kimoja cha kiada na kihakikiwe na wataalamu wa elimu ya juu, pia kiendane na muhtasari

v) Maeneo yenye utata katika mtaala yaboreshwe/kuwe na usawazisho wa maeneo yanayopingana katika vitabu

vi) Kuwe na semina za mara kwa mara ili kujenga uelewa wa pamoja

vii) Walimu wa Kiswahili washirikishwe katika kuandaa mitaala na mihtsari ya Kiswahili

viii) Kuwe na vitabu vyenye mada za isimu tu ili kuondoa mkanganyiko
ix) Kuwe na walimu wa kufundisha mada za isimu tu katika shule za sekondari
x) Vitabu vya kiada visiwe na mada ambazo hazimo katika muhtasari wa somo.

Kwa mujibu wa data toka maktabani, upungungufu huo pamoja na mapendekezo yamewahi pia kubainishwa na watafiti kadhaa, mfano Msanjila (kisha tajwa), alisema kuwa mada za sekondari hujirudia pasipo sababu ya msingi kiasi kwamba mwalimu asiye mzoefu huweza kurudia rudia kitu kilekile bila sababu yoyote. Naye Allwright (1981) anasema kuwa vitabu vya kiada katika mazingira fulani vinaweza kuathiri ushiriki wa mwanafunzi katika harakati za kujifunza. Mfano halisi ni vitabu ambavyo mada zake zimechanganywa. Warnings (1982) akimnukuu na Edge na Wharton (1998) na Tomlinson (2008) kuwa vitabu vya kiada yafaa viwe msaada kwa ajili ya mwalimu ambaye si mzoefu, au walimu wasio wazoefu katika ufundishaji wa lugha, hasa lugha ya mazungumzo. Majibu hayo ya watafitiwa yanajibu lengo namba tatu lililowataka watafitiwa wapendekeze njia zitakazorahisishia wanafunzi wanaohitimu somo la Kiswahili sekondari kujifunza somo la isimu vyuo vikuu.

## 4.5 Hitimisho

Utafiti huu ulibainisha kuwa katika muhtasari wa sekondari kuna mada ambazo humuandaa vema mwanafunzi atakayekwenda Chuo Kikuu baada ya kuhitimu Kiswahili sekondari aweze kumudu mada za isimu Chuo Kikuu; pia utafiti ulikusudia kubainisha kuwa kuna mada katika mtaala wa sekondari wa somo la Kiswahili ambazo hazimsaidii mwanafunzi atakayekwenda kusoma isimu Chuo Kikuu. Mada zote za aina mbili zimeweza kubainishwa kupitia utafiti huu. Pia utafiti

ulitaka kubainisha maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu mada za isimu zilizomo katika mtaala wa sekondari. Imebainika kwamba walimu na wanafunzi wana maoni hasi dhidi ya mada za isimu. Mwisho utafiti huu ulikusudia kubainisha njia za kupunguza au kuondoa vikwazo vinavyoweza kusababisha mwanafunzi atatizwe kusoma somo la isimu vyuo vikuu baada ya kuhitimu somo la Kiswahili katika elimu ya sekondari.  Njia muafaka za kupunguza vikwazo hivyo zimebainishwa kupitia utafiti hii.

# SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inahitimisha utafiti unaohusu “Tathmini ya mitaala ya Kiswahili kwa shule za sekondari Tanzania imuandaavyo mwanafunzi kumudu somo la isimu Chuo Kikuu”, sura imegawanyika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili inatoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sehemu ya tatu inaeleza mchango wa utafiti. Sehemu ya nne inaeleza mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kuhusu mitaala ya somo la Kiswahili sekondari hususani mada zinazohusiana na isimu na mielekeo ya wanafunzi na walimu na sehemu ya mwisho inapendekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi kutokana na mtafiti alivyobaini umuhimu wa maeneo hayo wakati wa utafiti.

### 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Katika kuchanganua data, mtafiti alitumia nadharia ya uamilifu ambayo iliasisiwa na Augute Comte (1787-1857), vilfredo (1848-1923), Herbert Spencer (1830-1903) na Emile Durkheim (1857-1917). Nadharia hii ilimsaidia mtafiti katika kufikia malengo yake yote matatu kwa kutumia mihimili mikuu miwili ya nadharia hii kama ilivyoainishwa katika sura ya pili.

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza mambo makuu manne:-

Kwanza, kuchunguza iwapo kuna mada za isimu katika muhtasari wa sekondari zinazomuandaa vema mwanafunzi atakayekwenda kusoma somo la isimu Chuo

Kikuu, pili kuchunguza mada katika muhtasari wa sekondari zisizo muandaa vema mwanafunzi atakayekwenda kusoma somo la isimu Chuo Kikuu, tatu, kuchunguza mielekeo hasi ya walimu na wanafunzi dhidi ya mada za isimu na nne, utafiti ulitaka kubainisha njia za kupunguza au kuondoa vikwazo vinavyoweza kusababisha mwanafunzi atatizwe kusoma somo la isimu vyuo vikuu.

Utafiti umeweza kuyafikia malengo yake ya jumla pamoja na malengo mahususi yaliyokusudiwa. Utafiti huu umefanyika katika Manispaa ya Tabora. Jumla ya watafitiwa 60 walishiriki katika utafiti huu wakiwemo wanafunzi na walimu wa shule za Sekondari Ipuli, Kazima, Kazehill, Kariakoo, Lwanzali, Nyamwezi na Kanyenye. Pia wanaChuo watano wa Chuo Kikuu cha AMUCTA walishiriki katika utafiti huu.

Data zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya hojaji, mahojianao na maktabani na zimechanganuliwa kwa mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi kwa lengo la kutoa taarifa inayojitosheleza.

Sura ya kwanza imetoa taarifa kuhusu mada ya utafiti, ikiwa ni pamoja na utangulizi wa jumla, tofauti ya mitaala na mihtasari vimeelezwa pia mada za Kiswahili isimu sekondari zimeorodheshwa. Tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na mipaka ya utafiti navyo vimefafanuliwa.

Sura ya pili imeeleza baadhi ya kazi zilizofanywa na wataalamu mbalimbali juu ya mitaala pamoja na kueleza kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu.

Sura ya tatu imefafanua namna utafiti ulivyofanyika. Sura imegawanywa katika sehemu zifuatazo:- Sehemu ya kwanza imeonesha eneo la utafiti, sehemu ya pili imefafanua kundi lengwa, sehemu ya tatu imeeleza sampuli ya utafiti na mchakato wa usampulishaji, sehemu ya nne imeeleza mbinu za kukusanyia na kuchanganua data, sehemu ya tano imeeleza vifaa vilivyotumika katika utafiti na sehemu ya sita imeeleza changamoto zilizojitokeza wakati wa kukusanya data.

Sura ya nne imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu na sura ya tano imetoa muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti. Sura imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza imetoa muhtasari wa utafiti mzima, sehemu ya pili imetoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu, sehemu ya tatu imeeleza mchango wa utafiti, sehemu ya nne imetoa mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kuhusu mtaala wa Kiswahili isimu kwa ngazi ya sekondari, sehemu ya tano imependekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi, na kisha hitimisho la sura nzima limetolewa.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

### 5.3.1 Kubainisha Mada Zinazomuandaa Vema Na Zisizomuandaa Vema Mwanafunzi Anayehitimu Kiswahili Sekondari Na Kwenda Kusoma Isimu Chuo Kikuu

#### 5.3.1.1 Katika Kujibu Lengo La Kwanza, Mofolojia Ilibainika Kuwa Na Mada Nyingi Tangulizi Katika Mtaala Wa Sekondari, Hivyo Kuwa Msaada Kwa Atakayekwenda Kusoma Isimu Chuo Kikuu

Utafiti huu umebaini kuwa zipo kozi za Chuo Kikuu za somo la isimu ambazo zina mada nyingi tangulizi ambazo ni msaada mkubwa katika mtaala wa Kiswahili wa sekondari Tanzania. Kozi ambayo ina mada nyingi tangulizi ni Mofolojia ya Kiswahili ambapo baadhi ya mada tangulizi zilizotajwa ni pamoja na mofimu, ngeli za nomino, matumizi ya o-rejeshi, aina za maneno, unyambulishaji, uundaji wa maneno na kadhalika.

#### 5.3.1.2 Imebainika Kuwa Zipo Mada Za Kiswahili Isimu Sekondari Zisizomuandaa Vema Mwanafunzi Wa Kiswahili Sekondari Kwa Ajili Ya Kusoma Somo la Isimu Chuo Kikuu

Utafiti huu umebaini kuwa zipo kozi za Chuo Kikuu za somo la isimu ambazo hazina mada tangulizi katika mtaala wa kiswahili wa sekondari Tanzania hivyo kuleta ugumu kwa mwanafunzi anayehitimu somo la Kiswahili sekondari na kwenda kusoma kozi ya isimu Chuo Kikuu. Kozi ambayo imetajwa kuwa haina mada tangulizi ni fonetiki ikifuatiwa na fonolojia. Watafitiwa walipendekeza kuwa yafaa mada hizo ziwe na mada za utangulizi pia kwa upande wa sekondari ili ziwaandae vema kusoma Chuo Kikuu somo la isimu.

#### 5.3.1.3 Mofimu Kama Istilahi Ya Kiisimu Haifasiliwi Sawa Sawa Sekondari

Watafitiwa walieleza kuwa fasili ya mofimu kwa sekondari ni tofauti na fasili inayotumika Chuo Kikuu.

Matokeo haya yanaungwa mkono na data toka maktabani ambapo, Mgullu (1999:123) anasisitiza kuwa mofu imekuwa ikichanganywa na mofimu kwa sababu

mofu ilianza kutumika baadaye zaidi karne ya 20 hasa baada ya kuasisiwa kwa sarufi zalishi. Watafitiwa walieleza kuwa fasili ya mofu katika ngazi ya Chuo Kikuu ndiyo fasili ya mofimu katika ngazi ya sekondari.

Watafitiwa wanaeleza kuwa mofimu ni dhana dhahania iliyomo akilini mwa mtu tofauti na elimu waliyoipata sekondari. Madai yao ni ya kweli kwa kuwa katika Kitabu cha Kiswahili kwa ajili ya kidato cha pili cha Ipara na wenzake (2011) wanafasili mofimu kuwa ni neno au sehemu ya neno inayobeba maana, naye Masebo (2007:137-167) katika kitabu cha Kiswahili kidato cha tano na cha sita, anafasili mofimu kuwa ni kipashio cha msingi katika Mofolojia ya lugha. Lakini kama tujuavyo sehemu ya neno siyo Mofimu bali ni mofu kama Mgullu (1999: 15) asemavyo kuwa mofimu ni dhana dhahania iliyomo akilini mwa watu na ambayo ni sehemu ya umilisi wa lugha wa kila mtu.

#### 5.3.1.4 Imebainika Kuwa Uchanganuzi Wa Tungo Unatofautiana Kutegemeana Na Watunzi Wa Vitabu, Hivyo Kutowaandaa Vema Wanafunzi Watakaokwenda Kusoma Isimu Chuo Kikuu

Watafitiwa walidai kuwa mada ya uchanganuzi wa tungo hutofautiana kutoka kitabu kimoja hadi kingine. Madai yao yana ungwa mkono na Massamba (1999:48) anaposema kuwa "tukiachia matatizo mengine yanayojitokeza katika kitabu hicho (yaani kitabu cha Nkwera), kuna tatizo kubwa la kuchanganya mikabala ya uchanganuzi ambayo haiendani". Massamba na wenzake wanaendelea kueleza kuwa, kwa mujibu wa Nkwera katika daraja la kwanza Sentensi ina Kiima (K) na Kiarifu (A); katika daraja la pili sentensi ina Kundi Nomino (KN), Fungu Tenzi (FT),

Shamirisho (Sh) na Chagizo (Ch). Hapa ni dhahiri kwamba Nkwera anachanganya dhana za sarufi za kimapokeo na Sarufi Msonge ambazo zinatumia Kiima, Kiarifu, Shamirisho na chagizo, na dhana za Sarufi Miundo Virai ambayo hutumia istilahi za kundi Nomino na kundi Tenzi." Ni hakika kuwa mada au kipengele cha mada inayowachanganya wanafunzi kupitia vitabu vya kiada au rejea haiwezi kusemekana kuwa ina waandaa vema. Kielelezo kifuatacho kinadhihirisha mikanganyiko hiyo ambapo tungo moja imeonekana kuchanganuliwa kwa njia tofauti kama inavyooneshwa katia 5.1(a) na 5.1(b).




5.1(a) Chanzo: John (2009)

Kama tungo hiyo hapo juu ingechanganuliwa katika ngazi ya elimu ya Chuo Kikuu ingeoneshwa kama ifuatavyo:-




5.1(b)

Katika kielelezo 5 (a) tunaona akitumia istilahi za Kiima na kiarifu na katika Kielelezo (b) tunaona $S_2$ ikitumika badala ya KTg, pia katika mfano 5(a) tunaona uchanganuzi ukitumia Kiima na Kiarifu na mfano 5 (b) umetumia Kikundi Nomino na Kikundi Tenzi. Massamba (1999) anasema kuwa hapa ni dhahiri kwamba kuna uchanganyaji wa dhana za sarufi za kimapokeo na Sarufi Msonge ambazo zinatumia Kiima na Kiarifu, na dhana za Sarufi Miundo mkabala ambao hutumia KN na KT.

#### 5.3.1.5 Imedhihirika Kuwa Mada Ya Kamusi Sekondari Hufundishwa Bila Kamusi, Hivyo Kutomuandaa Vema Mwanafunzi Atakaye Soma Isimu Chuo Kikuu

Kutokana na uhaba mkubwa wa kamusi uliobainika katika shule za sekondari ni kwamba mada ya kamusi imebainika kuwa hufundishwa bila uwepo wa kamusi.

Shule nyingi zilibainika kuwa na kamusi moja na watafitiwa walikiri kuwa kamusi hutumika kwa dharura shuleni. Mada inayofundishwa bila zana anuawai za kufundishia haiwezi kumuandaa vema mwanafunzi atakayekwenda kusoma isimu Chuo Kikuu.

#### 5.3.1.6 Uhaba wa Vitabu vya Kiada Shuleni ni Kikwazo Katika Kuwaandaa Vema Wanafunzi wa Sekondari Watakaokwenda Kusoma Isimu Chuo Kikuu

Kati ya shule 07 ziilizofanyiwa utafiti ni shule 02 tu zilizodai kuwa na vitabu vya rejea, japo idadi yake haikuweza kubainika. Shule nyingine tano sawa na 71.4% hazikuwa na vitabu vya rejea. Ilibainika kuwa uwiano wa vitabu vya Kiswahili ambavyo ndani yake hujumuishwa mada za isimu ulikuwa 1:5-10. Upungufu mkubwa wa vitabu vya somo ni ishara mojawapo ya viongozi wa shule kutothamini somo husika kama Msanjila (2005) asemavyo kuwa somo la Kiswahili halitengewi fedha nyingi kama yalivyo masomo ya sayansi. Tomlison (2008) anasema kuwa vitabu vya kiada yafaa viwe msaada kwa mwalimu ambaye si mzoefu. Katika mazingira yasiyo na vitabu vya isimu si rahisi kusema kuwa mwanafunzi anayesoma katika ngazi hiyo ya elimu ya sekondari atakuwa ameandaliwa vema.

#### 5.3.1.7 Utafiti Umethibitisha Kuwa Sentensi Katika Vitabu Vya Kiada Vya Sekondari Huainishwa Bila Ruwaza Mahususi

Watafitiwa walidai kuwa uainishaji wa aina za sentensi hufanyika kutegemeana na mtunzi wa kitabu. Wapo wanaotambua sentensi sahili, ambatano, changamano, na

wengine huongeza sentensi arifu, shurutia, amrishi, swalifu, na mshangao bila ufafanuzi wowote.

Ilivyo ni kwamba vitabu hivyo vinapaswa kuainisha sentensi kwa kutumia kigezo kinacho julikana badala ya vitabu hivyo kuzigawa kiholela. Katika uainishaji wa sentensi Matinde (2012:158-160) amefafanua kuwa sentensi huainishwa kwa kuzingatia ama uamilifu wake au muundo wake. Mwanafunzi hawezi kuandaliwa vema kumudu kozi za isimu vyuo vikuu kama alijifunza kwa kutumia vitabu vyenye mkanganyiko sekondari.

### 5.3.2 Maoni Hasi Dhidi Ya Mada Za Isimu Kwa Wanafunzi Na Walimu Wa Sekondari Pamoja Na Wanafunzi wa Chuo Kikuu

#### 5.3.2.1 Mada Za Isimu (Sarufi Na Utumizi Wa Lugha) Sekondari Hazina Alama Nyingi Kwenye Mitihani Ya Mwisho ya Kitaifa

Imebainika kuwa wanafunzi wengi na walimu hawakazanii zaidi mada za isimu kwa kuwa hazina alama nyingi katika mitihani ya kitaifa kama ilivyo mada ya fasihi. Lengo kubwa la mwanafunzi kujifunza mada yoyote huwa ni kufaulu mitihani kama asemavyo Kimani anapowanukuu wataalamu Gathumbi na Masembe (2005) kuwa wanafunzi wengi huimarisha lugha tu kwa minajili ya mitihani na wakisha kuifanya mitihani hiyo hupuuzilia mbali kanuni faafu za lugha hiyo na hata kuichukulia kama wasiyoielewa kabisa. Naye Arends (1997) anaeleza kuwa ufaulu katika taaluma hupatikana kupitia mitihani na majaribio ya masomo mbalimbali. Kwa mantiki hiyo walimu na wanafunzi wamejenga mielekeo hasi dhidi ya mada za isimu na utumizi wa lugha kwa kuwa hazina motisha kubwa ya alama katika mitihani ya mwisho.

#### 5.3.2.2 Kuna Maoni Hasi Kuwa Mada Za Isimu Ni Ngumu

Watafitiwa wa makundi yote walibainika kuamini kuwa mada za isimu ni ngumu, imani ambayo haijulikani chanzo chake japo walitaja kuwa mada kama fasihi inafurahisha, kuelimisha na ina matumizi ya kila siku katika maisha halisi ya kijamii. Imani potofu ya mada au somo husababisha ufaulu duni kwa wanafunzi kama walivyo bainisha Mbunda (1979) na Seka (1979). Pia Muhochi (2010 ) katika makala iitwayo *mielekeo ya wasomi wa kiswahili na viongozi wa Afrika mashariki kuhusu lugha ya Kiswahili* akiwanukuu watafiti mbalimbali anasema, utafiti uliofanywa na Clement, Major, Gardner na Symthe katika mwaka wa 1977 (Gardner 1985) uligundua kwamba kuna uhusiano kati ya sifa za kimielekeo na motisha, na matumizi ya lugha. Katika kila hojaji iliyowataka waoneshe upenzi wao baina ya mada za isimu na zisizo za isimu ilibainika kuwa watafitiwa wanapenda zaidi mada zisizo za isimu (ona kielelezo namba 4.5).

#### 5.3.2.3 Maoni Hasi Kuwa Mada Za Isimu Hazihitaji Kusomwa Kwa Muda Mrefu

Mwelekeo hasi wa kutopenda kujisomea mada za isimu sekondari ulipimwa kwa muda wanaotenga wanafunzi kusoma mada mbalimbali za kiswahili. Ilibainika kuwa walikuwa wakitumia muda mwingi zaidi kusoma riwaya na tamthiliya kuliko mada zinazohusiana na isimu. Walipoulizwa sababu za kutenga muda mwingi kwenye mada waliyo chagua (riwaya na tamthiliya) walisema mada za ismu hazihitaji kusoma sana. Mwelekeo hasi wa namna hii hauwezi kuwaandaa vema kusoma somo la isimu Chuo Kikuu maana maandalizi yao kwa ajili ya kusoma isimu tangu sekondari hayatoshi.

### 5.3.3 Maoni Kuhusu Namna Ya Kupunguza Matatizo Ya Kujifunza Mada Za Isimu Sekondari Kwa Ajili Ya Kurahisisha Kusoma Kozi Ya Isimu Chuo Kikuu

Watafitiwa walipendekeza njia mbali mbali ambazo zinaweza kupunguza matatizo ya ujifunzaji wa mada za isimu sekondari ili kurahisisha usomaji wa kozi ya isimu Chuo Kikuu. Yafuatayo ni mapendekezo waliyo yatoa:-

i) Mada za isimujamii na fonetiki ziingizwe katika mtaala wa sekondari kwa kiasi cha kuweza kumsaidia mwanafunzi atakaye kwenda kusoma isimu Chuo Kikuu.

ii) Vitabu vinavyoshughulikia isimu tu viandaliwe kwa ajili ya shule za sekondari.

iii) Maabara za lugha ya Kiswahili zianzishwe.

iv) Mada zipangwe vizuri na kwa kufuata vidato.

v) Kwa baadhi ya mofimu, mipaka baina ya mofimu haiko wazi, tahajia zibadilishwe.

vi) Kuwepo na kigezo maalumu cha kutambua aina za sentensi.

vii) Kuwe na kigezo kimoja cha upatikanaji wa ngeli za nomino.

viii) Kuwe na kitabu kimoja cha kiada na kihakikiwe na wataalamu wa elimu ya juu, pia kiendane na muhtasari.

ix) Maeneo yenye utata katika mtaala yaboreshwe/kuwe na usawazisho wa maeneo yanayopingana katika vitabu.

x) Kuwe na semina za mara kwa mara ili kujenga uelewa wa pamoja.

xi) Walimu wa Kiswahili washirikishwe katika kuandaa mitaala na mihtsari ya somo hilo.

xii) Yaliyomo katika mihtasari ya somo yaoane na yaliyomo katika vitabu vya kiada.

xiii) Mada za isimu zisijirudie katika vidato tofauti bila sababu ya msingi.

xiv) Kuwe na walimu wa kufundisha mada za isimu tu katika shule za sekondari.

xv) Kuwe na kamusi na vitabu vya kiada vya kutosha shuleni.

Mapendekezo hayo yamewahi pia kubainishwa na watafiti kadhaa, mfano Msanjila (kisha tajwa), alisema kuwa mada za sekondari hujirudia pasipo sababu ya msingi kiasi kwamba mwalimu asiye mzoefu huweza kurudia rudia kitu kilekile bila sababu yoyote. Warming (1982) anasema kwamba vitabu vya kiada ni chanzo muhimu kwa mwanafunzi shuleni kwa ajili ya kujifunza, kueneza utamaduni, na kuongeza maarifa ya wanafunzi. Warning akiwarejea Edge na Wharton (1998) na Tomlinson (2008) anasema kuwa vitabu vya kiada yafaa viwe msaada kwa ajili ya mwalimu ambaye si mzoefu, au walimu wasio wazoefu katika ufundishaji wa lugha, hasa lugha ya mazungumzo.

Kuokana na muhtasari uliotolewa hapo juu, ni dhahiri kuwa malengo yote matatu ya utafiti huu yamefikiwa pasipo shaka yoyote.

## 5.4 Mchango wa Utafiti

Matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu yatasaidia kutoa mchango wa maendeleo ya mada za isimu na somo la isimu kwa ujumla kwani utafiti huu umebaini upungufu uliomo katika mitaala, mihtasari na vitabu vya kiada ambayo yafaa yafanyiwe kazi na wadau mbalimbali. Aidha, utafiti huu umebainisha mada za isimu sekondari zenye

msaada na zisizo na msaada kwa mwanafunzi anayehitimu sekondari na kisha kujiunga na somo la isimu Chuo Kikuu.

Pia utafiti huu umebaini mielekeo hasi ya wanafunzi na walimu dhidi ya mada za isimu na Kiswahili kwa ujumla. Pia utafiti huu umeorodhesha mapendekezo ya watafitiwa kuhusu njia muafaka za kuboresha ujifunzaji ulio bora wa mada za isimu sekondari ili wahitimu wa somo la Kiswahili sekondari waweze kujifunza somo la isimu Chuo Kikuu kwa urahisi.

Vilevile utafiti huu unaweza kutumika kama ni marejeo kwa tafiti za baadaye. Halikadhalika, utafiti huu unatoa mwanga na kuiweka makini jamii ya wanaisimu, waandaaji wa mitaala, Baraza la mitihani la Tanzania, watunzi wa vitabu vya kiada na rejea kuwa kuna maswala yanayogusa taasisi zao au kazi zao hivyo yafaa wayarekebishe kwa ajili ya maendeleo ya somo la isimu Tanzania na duniani kwa ujumla.

## 5.5 Mapendekezo

Mapendekezo yote ya watafitiwa yameorodheshwa katika sehemu ya 5.3.3 hapo juu. Hata hivyo mtafiti anapendekeza yafuatayo kwa mamlaka zinazohusika kutokana na data iliyo changanuliwa:

i) Baraza la mitihani la Tanzania lisawazishe alama katika mada zote za somo la Kiswahili sekondari ili kuondoa tatizo la alama nyingi kuelemea upande wa fasihi.

ii) Mada ambazo zimebainika kuwa hazina utangulizi mzuri sekondari ziongezewe mada za utangulizi kwa ngazi ya sekondari.

iii) Wanafunzi wajengwe kisaikolojia ili wawe na mielekeo chanya dhidi ya mada za isimu.

iv) Pendekezo la (iii) hapo juu litawezekana ikiwa kutakuwa na walimu wanaofundisha isimu pekee sekondari; hivyo kuwe na walimu wa isimu tangu ngazi ya sekondari.

v) Vitabu vya kiada vinavyokinzana vibainishwe na kurekebishwa.

## 5.6 Tafiti Fuatishi

Utafiti huu umechunguza "Tathmini ya mitaala ya kiswahili kwa shule za sekondari Tanzania imuandaavyo mwanafunzi kumudu somo la Chuo Kikuu". Mtafiti anapendekeza maeneo yafuatayo yafanyiwe tafiti ili kuendeleza matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu:

i) Watafiti wengine wafanye utafiti kama huu katika eneo la utafiti tofauti na kwa kiunzi cha nadharia tofauti ili kubaini kama watapata matokeo kama haya yaliyopatikana.

ii) Watafiti waendelee kuchunguza sababu zinazo sababisha wanafunzi na walimu wawe na mtazamo hasi dhidi ya mada za isimu na somo la Kiswahili kwa ujumla.

iii) Ipo haja kwa watafiti kuchunguza mada muhimu tangulizi zinazoweza kuingizwa katika mtaala wa sekondari ili zimsaidie mwanafunzi atakaye kwenda kusoma isimu vyuo vikuu.

iv) Tafiti fuatishi zichunguze ili kubainish mada ambazo zimo katika vitabu vya kiada lakini hazimo katika mihtasari ya Kiswahili sekondari.

v) Watafiti wapya wanaweza pia kuchunguza kama kwa ngazi ya sekondari kutakuwa na walimu wa mada za isimu tu, hali hiyo itaondoa mtazamo hasi dhidi ya mada za isimu.

vi) Utafiti zaidi unahitajika kubaini kama ni kweli kwamba mada zote za Kiswahili sekondari zikitengewa alama sawa katika mitihani ya taifa, basi hatua hiyo itawafanya wanafunzi wapende na kufaulu zaidi mada za isimu.

vii) Tafiti zijazo zichunguze chanzo cha mitazamo hasi ya walimu na wanafunzi dhidi ya mada za isimu.

Tafiti zilizopendekezwa katika sehemu hii zikitekelezwa pamoja na utafiti huu zitakuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza taaluma ya isimu Tanzania na duniani kwa ujumla.

## 5.7 Hitimisho

Sura hii imehitimisha utafiti unaohusu “Tathmini ya mitaala ya Kiswahili kwa shule za sekondari  nchini Tanzania imuandaavyo mwanafunzi kumudu somo la Isimu Chuo Kikuu”. Sehemu ya kwanza imeoa utangulizi wa sura hii; kisha muhtasari wa utafiti mzima umetolewa. Sehemu ya pili imetoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sehemu ya tatu imeeleza mchango wa utafiti. Sehemu ya nne imeeleza mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kuhusu malengo ya utafiti na sehemu ya mwisho imependekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

## MAREJELEO

Allright, R. L. (1981). What do we want teaching materials for? *ELT Journal,* 36 (1), 5-18.

Babusa, H. (2010). Uchanganuzi Linganuzi wa Mielekeo na Umilisi wa Lugha ya Kiswahili wa Wanafunzi Katika Mikoa ya Pwani na Nairobi Nchini Kenya. Unpublished PhD. Thesis. Kenyatta University.

Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa lugha na isimu*. Dar-res-Salaam: Dar-es-Salaam University Press:

Brown, H. D. (2007). *Principles of Language Learning and Teaching* (5th Ed.). New York: Pearson Education White Plains

Buliba na wenzake (mwaka haujulikani). *Misingi ya Nadharia na mbinu za utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational publishers.

Celce-Murcia, M. (1991). *Grammar Pedagogy in Second and Foreign Language Teaching*. New York: Newburry House.

Cohen, L. (1980). *Research methods in Education (5th edition).* London: Rutledge. Falmer.

Enon, C. J. (1995). *Educational Research, Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.

